# Hati ya Ruhusa ya Ziara za Kimasomo

Ziara ya kimasomo kwenda ______________________________ inapangwa ______________________ na
(Tarehe)
____________________________________. Ziara itaanza saa _________________________________
(Muda)
na darasa litarudi shuleni takribani ____________________________________.
(Muda)

Wanafunzi watasafiri kwa: ■ basi la shule ■ gari binafsi ■ kutembea.

Tungependa mtoto wako ashiriki kwenye ziara husika. Hata hivyo, bila idhini yako ya maandishi hataruhusiwa kuhudhuria. Tutaweka mipango mingine kwa ajili ya mtoto wako shuleni. Tafadhali jaza fomu hii na uirejeshe shuleni ikiwa unatoa ruhusa kwa mtoto wako kwenda katika ziara hii ya kimasomo.

Gharama ya ziara hii ya kimasomo ni $__________. Ziara za kimasomo ni tukio muhimu kwa wanafunzi wetu. Hakuna mwanafunzi atakayetengwa kwa msingi wa kukosa uwezo wa kulipia ziara. Ikiwa unahitaji usaidizi, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako au mkuu wa shule. Sera ya bodi ya shule inakataza kunyimwa haki ya kushiriki katika ziara za kimasomo kwa msingi wa kukosa uwezo wa kulipia.

**Ili mzazi/mlezi ahudhurie ziara ya kimasomo, lazima awe amewasilisha ombi la kujitolea na kupewa kibali cha kujitolea katika Wilaya ya Shule ya Lansing.**

---

## Ruhusa ya Mzazi/Mlezi

Natoa ruhusa kwa ________________________________________ kuandamana na darasa lake kwenye ziara ya kimasomo inayopangwa mnamo _______________. Tunaelewa taratibu husika na tunaamini kwamba tahadhari na mipango muhimu ya uangalizi na usimamizi wa wanafunzi wakati wa ziara itazingatiwa.

_________________________________ _____________________ _____________________

Saini ya Mzazi/Mlezi Tarehe Nambari ya simu

_________________________________

Jina kwa Herufi Kubwa

■ Napatikana na nipo tayari kuwa kiongozi wa ziara hii ya kimasomo.

# Matumizi ya Gari Binafsi kwa Ziara za Kimasomo

**Masharti ya Kusafiri kwa Gari Binafsi**

Katika baadhi ya matukio, inaweza kuwa muhimu kutumia madereva wa kujitolea na magari binafsi kwa ziara ya kimasomo. Katika hali kama hizo, taratibu zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa:

1. Weka ukomo wa idadi ya abiria wanaopangwa kwa kila gari kulingana na uwezo wa mkanda wa kiti wa gari. Hakikisha kwamba abiria wote wamefunga mikanda ya usalama.
2. Andaa orodha ya abiria waliopangwa kwa kila gari. Nakala moja ya orodha apewe dereva na nakala moja inawekwa katika faili la ofisi kuu.
3. Andaa njia husika kwa ajili ya kila gari kuifuata wakati wa ziara ya kimasomo na uhakikishe kuwa kila dereva anaifahamu njia hiyo.
4. Hakikisha kila dereva ana nakala ya maelezo ya dharura.
5. Shauri madereva wa kujitolea kukagua bima yao ili kuhakikisha kwamba wana bima ya kutosha kwa hatari zinazohusika.
6. Kila dereva anatakiwa kujaza na kusaini taarifa ifuatayo ambayo itawekwa kwenye faili katika ofisi ya shule.

**MUHIMU:**
**Tafadhali kumbuka kuwa sheria ya Jimbo la Michigan kwa sasa inahitaji kuwa mzazi yeyote anayemwendesha wanafunzi kwenye ziara ya kimasomo katika gari lake binafsi LAZIMA awe na kiti maalum chenye mkanda wa begani kwa kila mwanafunzi aliye chini ya miaka 8 au urefu wa 4'9".**

Nathibitisha kwamba nina leseni ya udereva iliyo halali, na isiyo na vikwazo,

# ________________________________ na kwa ufahamu wangu, sasa hivi

nina pointi ______ kwenye rekodi yangu.

Naamini gari naloliendesha katika ziara hii lipo katika hali salama ya kufanya kazi.

Nimezungumza na kampuni yangu ya bima na nina bima ya kutosha kwa hatari zozote zinazohusika.

Saini ____________________________________________Tarehe ____________________